

LEARNING BY EAR 2010
SHALL I TELL YOU SOMETHING?
AFRICAN FABLES FOR A CULTURE OF PEACE

EPISODE 07: „DIKUM DAKUM, THE MAGIC SPELL”

AUTHOR: IBRAHIMA NDIAYE
**EDITORS: YANN DURAND, STEFANIE DUCKSTEIN,
NAÏMA GUIRA**
TRANSLATION: NATALIE GLANVILLE-WALLIS
PROOFREADING: TONY DUNHAM
KISUAHELI : ERIC PONDA

Sound Clips: liegen bis Mitte Juli vor

CHARACTERS:

1. NARRATOR (male, 40 years old at least)
2. ELEPHANT (male, around 40 years old)
3. SIMBA THE LION (male, about 30 years old)
4. CHAMELEON STAMMERING (female, around 20 years old)
5. HYENA (female, around 20 years old)
6. MAMA TENGA, OLD WOMAN (female, sounding +/- 70 years old)

VOICE FOR MONKEY NEEDED, BUT ONLY FOR A CRY (p. 5, n°20)

INTRO:

Hujambo na karibu kwa makala ya saba kwenye mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo jenga Maisha yako, tukiwa bado katika masala ya Ngano, maada kuu ni “JE NIKUDOKEZEE” Ngano za utamaduni wa Mwafrika kuhusu mbinu za kudumisha amani na maridhiano .”Hii leo tunaungana na rafiki zetu Wanyama wakiwa katika juhudi zao za kutafuta chakula wakati wa kiangazi, na wanajifunza mbinu mbali mbali za kukabiliana na hali hiyo. Hivyo endelea kuwa nasi hadi mwisho wa kipindi ufahamu iwapo wanafaulu au la katika hadhithi hii ya “Miujiza ya Dikum Dakum”.

1. MUSIC (play as background for the entire script)

2. NARRATOR:

Hapo zamani za kale katika nchi moja iliyojulikana kama Kabwana, kulitokea kiangazi cha kutisha, kiangazi ambacho hakikuwahi kushuhudiwa katika historia ya nchi hiyo. Na kadri kiangazi hicho kilivyozidi, ndivyo wanyama nao walivyoendelea kukabiliwa na tisho la kuangamia. Chakula kilikuwa haba na hakukusalia chochote. Siku moja Ndovu aliitisha mkutano wa wanyama hao, mkutano uliofanyika chini ya mbuyu mkubwa, kujadilia suala hilo. Na kwa vile ndiye aliyekuwa mzee kuliko wote, Ndovu aliwahutubia...

3. ELEPHANT:

“Ndungu zanguni, nashukuru kwa kuitikia mwito huu. Kama mjuavyo, hali ya kiangazi inazidi kutuathiri nchi yetu. Iwapo hatutajitolea na kushirikiana kurekebisha hali hii, basi huenda sote tukaangamia. Na mimi nina pendekezo moja hapa. Kesho alfajiri sote tutaandamana kutafuta chakula. Na tutakapopata chakula cha kututosha, tutagawanya sawa kama ndugu!”

4. NARRATOR:

Wazo hilo liliridhiwa na wanyama wote na asubuhi na mapema kundi hilo la wanyama likianza safari.

5. ELEPHANT, LION, BIRDS: Sounds of animals (elephant trumpeting, lion roaring, birds chirping and flying, heavy and light steps)

6. NARRATOR:

Simba, mfalme wa wanyama wote, aliwaongoza wenzake, huku Ndovu akisalia nyuma akiandamana na Twiga aliyekuwa amembeba Kinyonga mwenye jicho pevu. Kinyonga huyo alijishikilia kwa makini katikati ya mashikio ya Twiga. Simba alikuwa amemuagiza kuangalia huku na huko na kuwapasha habari punde tu anapona shamba la matunda.

Safari hiyo ilikuwa ya mwendo mrefu huku jua likiwaka sana. Lakini msafara wao ukakumbwa na matatizo pale Fisi alipoanza kulalama kutokana na uchovu.

7. HYENA (exhausted):

“Puh, siwezi kuendelea na safari , hebu tupumpuzike ”

8. NARRATOR:

Matamshi hayo yalimkasirisha sana Simba, aliyeanza kutokwa na subr na kumjibu kwa ukali.

9. SIMBA THE LION: *Roar*

10. SIMBA THE LION (*angry*):

“Tosha sasa tumesikia, hakuna haja ya kuendelea kunung’unika!
Pia una uhuru wa kurudi nyumbani, lakini kumbuka utarudi peke
yako!”

11. NARRATOR:

Na ghafla Kinyonga akatoa sauti kubwa.....

12. CHAMELEON (*excited, stammering*):

“Wow, wow, wow! Na...Na Naona mti mkubwa wenye majani
ya kibichi na matunda ya rangi ya kijani kibichi, manjano na
mekundu. Nadhani ni mti wa Ma..Ma..Marula”

13. NARRATOR:

Wote wakashikwa na hamu kubwa, wasiamini waliyokuwa
wakiambiwa na kinyonga.

14. ALL OTHER ANIMALS (*excited*):

“Una hakika?”

15. NARRATOR:

Kana kwamba ameudhika na matamshi hayo, alijibu kwa kigugumizi:

16. CHAMELEON (offended, stammering):

“Ya...yaa...yaa...yaani ha...ha... hamuamini macho makali ya Kinyonga sivyo? Basi endeleeni na njaa zenu!”

17. NARRATOR:

Hapo Simba akaamuru kikosi cha wanyama kuelekea moja kwa moja katika sehemu walikoelekezwa na Kinyonga ili kudhibitisha habari hizo. Na kila mmoja akaanza kufurahia habari hizo njema. Kweli Kinyonga alikuwa na macho makali kwani Mti aliouona ni ule wa Marula ukiwa umetanda matunda.

Hivyo msafara kwa taratibu ukaeleka kwenye mti huo. Kisha wanyama wote wakauzingira huku mate yakiwadondoka. Hata fisi aliyekuwa akilalamika pia alichangamka.

Ndovu alianza kupanga utaratibu wa kuvuna matunda hayo kwa furaha sana.

18. ELEPHANT (happy):

“Tumbili sasa shika usukani, tunataka upande juu ya mti na kutunda matunda yote.”

19. NARRATOR:

Kwa wepesi wake Tumbili alipanda mti na kuanza kutingisha kila kitagaa lakini wapi, hakuna tunda lililoanguka ng'o! Ndovu kwa ubabe wake alishikwa na hasira na akaanza kutumia mkonga wake kutingisha mti mzima lakini pia hakuna tunda hata moja, isipokuwa Tumbili tu aliyekuwa juu ya Mti ...

20. MONKEY: Cry of monkey falling and crash landing sound

21. NARRATOR

Ndovu alizidi kupandwa na hasira na akatoa mlio uliowatisha wanyama wengine wote.

22. ELEPHANT (angry):

“Huu mti umelogwa. Sasa utanijua mimi ni nani...”

23. NARRATOR:

Lakini ghafla Kinyonga akasema;

24. CHAMELEON

“Hebu ngoja kidogo Ndovu. Kwa umbali naweza kuona Mbuyu... na chini yake namuona Mama mzee ameketi. Nadhani anakula matunda haya haya!”

25. ELEPHANT

“Hebu subirini hapa. Nitaenda kumhoji Mama huyo!”

26. NARRATOR

... akajibu ndovu huku akielekea moja kwa moja hadi kwenye mbuyu alikoelekezwa !

27. ELEPHANT RUNNING

28. ELEPHANT

“Habari Mama, samahani kwa kukusumbua, lakini nilitaka kukuuliza wapi umeyapata matunda hayo mazuri unayokula. Mimi na rafiki zangu tunatapatapa kwa njaa...”

29. NARRATOR:

Ndovu alianza kuelezea masaibu waliyopitia na kisha kumfahamisha mama huyo jinsi wanyama wengine walivyokuwa wakihangaika kutafuta chakula. Mama Tenga aliwaonea huruma sana wanyama hao.

30. MAMA TENGA:

“Mimi nimeujua mti ule kwa zaidi ya miaka 100 sasa! Ni mti wenye matunda matamu sana. Lakini huwezi kuyatunda bila ya kusema maneno haya ya miujiza: **(cheerfully pronounced)**
Dikum dakum lakum dinikum fankum fankum bibi saya.”

31. NARRATOR:

Ndovu alimshukuru sana mama huyo na kama ilivyo kawaida yale akainua mkonga wake na kutoa sauti kubwa huku akirudi kwa wenzake.

32.ELEPHANT trumpeting

33. NARRATOR:

Mama Tenga alimtazama akiondoka huku akimchekelea kwa stizai. Akiwa njiani Ndovu alirudia maneno aliyoambiwa asije akasahau. Lakini alipofika tu mahala walipokuwa wanyama wenzake, maneno yote aliyokuwa ameambiwa yakawa yamemtoka. Hali iliyozua vurugu baina yao. Ndovu aliinua kichwa huku akiwa amechanganyikiwa kabisa.

34. ELEPHANT

“Kwanza tunahitaji kujua maneno ya siri. Yule mama mzee ameniambia lakini sasa nimeyasahau. Sijui nina shida gani...Mimi si mtu wa kusahau sahu mambo, na sijui leo imekuwaje.”

35. SFX: Murmur of disapproval from the crowd (*played by actors*)

Fisi aliyekuwa na njaa kupindukia, hakutaka kusikia chochote na akaanza kumkemean Ndovu:

36. HYENA

“Haiwezekani! Wewe unatudanganya. Nina wasiwasi kwamba labda unataka sisi tuondoke na kisha uyale peke yako matunda haya. Kwanza wewe huna kumbukumbu yoyote kama unavyodai! Sijui ni uji au ni ubongo ulioko kwenye kichwa chako. Wewe ni mwepesi sana wa kusahau mambo!”

37. NARRATOR:

Fisi huyo bila ya hata kuona haya, akatangaza kwamba anataka kwenda yeye binafsi kwa mama huyo kupewa maneno ya siri. Na bila ya kupoteza muda akaanza safari, huku akichechemea kuelekea kwa Mama Tenga. Baada ya kujifunza maneno hayo alirudi upesi kwa wenzake. Alikuwa na furaha isiyo kifani kutaka kudhihirisha ushujaa wake na kumdhihaki rafiki yake Ndovu.

Njiani alikuta mzoga wa Ngamia na bila ya kusita akauvamia mzoga ule na kuanza kuguguna kila mfupa. Aliposhiba akawa pia maneno aliyoambiwa na Mama Tenga yamemtoka.

Marejeo ya Fisi yule katika mkusanyiko wa wanyama wenye njaa kupindukia, hayakuleta faraja yoyote. Walianza kumtusi na kumlimbikizia lawama. "Hata wewe ni bure kabisa," wakamkemea. Wakati hayo yakijiri, Kifaru na Pundamilia walimnusa Fisi. "Umetusaliti. Hatuwezi tena kukuamini," akasema Kobe.

Fisi hakutikisika na lawama hizo.

38. HYENA

"Sawa nenda wewe basi tuone kama mambo yatanyoka. Wewe ni debe tupu tu!"

39. NARRATOR:

Na hapo wazo likamjia ndovu:

40. ELEPHANT *trumpeting*

41. ELEPHANT

“Tosha, tosha, hebu punguzeni hasira zenu! Hiyo haiwezi kutusaidia. Kama nakumbuka vizuri maneno hayo ya siri ni manane, hivyo tutabuni kamati nane na kisha kwenda moja kwa moja hadi kwa mama Tenga. Kila kamati itakuwa na jukumu la kushika na kukumbuka neno moja.”

42. SIMBA THE LION:

“Kweli hilo ni wazo zuri sana Ndovu.”

43. NARRATOR:

... Kila mmoja alimpongeza Ndovu na wote wakakubaliana kwa kauli moja na kisha kuanza safari hadi kwa Mama Tenga. Walipofika, wanyama hao walimrai Mama Tenga kuwafunza tena maneno hayo na kila kamati kushika neno moja. Waliporejea kwenye mti ule kila kamati ilitamka neno lake.

44. *Different groups of animals, one after another:*

“Dikum dakum lakum dinikum fankum fankum bibi saya.”

45. SFX: *Avalanche of fruits*

46. *ELEPHANT, LION, BIRDS, MONKEY: cries of surprise and joy (elephant trumpeting, lion roaring, birds chirping, monkey screaming etc.)*

47. NARRATOR:

Na ghafla matunda yakaanza kuanguka kwa fujo huku wanyama hao wakianza kusherehekea. Walikula shibe yao na kubeba ya kuwatosha waliporejea nyumbani.

Waliporudi nyumbani jioni hiyo, walikoka moto na wote kukusanyika nje kusherehekea mavuno hayo. Na hapo Simba mfalme akawashukuru kwa umoja wao.

48. *ELEPHANT, LION, BIRDS, MONKEY: Cries of joy (elephant trumpeting, lion roaring, birds chirping, monkey screaming etc.)*

49. SIMBA THE LION

“Sasa mnaona rafiki zangu, iwapo tutaendelea kushirikiana namna hii basi tunaweza kutatua matatizo yote yanayotukabili. Kweli Ndovu wewe unaweza kuwa mtetezi mashuhuri, Kinyonga una macho makali kama darubini, na wewe Fisi unanuka kama”

50. SFX: *Laughing crowd (played by actors)*

51. SIMBA THE LION

“Sasa kuna maana gani kwa mnyama kuwa na sifa ambayo haiwezi kumsaidia binafsi, bila ya ushirikiano wa wanyama wengine? Ni bora kuweka chini vichwa vyetu na kushirikiana katika kufanikisha malengo yetu? Katika siku sijazo, tunapasa kushirikiana na kuwa na umoja rafiki zangu!

52. NARRATOR

Na hadi hapo ngano yetu inafika ukingoni, na wa kwanza kuvuta harufu yake, bila shaka ataiona mbingu.

53. Music

OUTRO:

Naaaam! Basi kile kilichoonekana kuwa mwanzo mbaya, hatimaye uligeuka kuwa mwisho mwema. Na kwa maneno hayo ya siri ya Mama Tenga “Dikum Dakum”, ndipo tunafika mwisho wa makala yetu ya Noa Bongo hivi leo tukitumai kwamba, ujumbe huu umekufikia mpenzi msikilizaji. Kwamba bila ya kujali ubabe wako kama ndovu, ujasiri na jicho pevu kama Kinyonga, ufahamu pasipo na ushirikiano ni kazi bure, kwani umoja unaweza kuleta mabadiliko katika ulimwengu huu tunamoishi. Na hata kama wewe ni mtu wa kunung'unika au mlahi kama fisi pia unaweza kubadilika na kuchukua jukumu. Tungependa kusikia maoni yako pia msikilizaji. Je, umewahi kujikutaka katika hali ambapo juhudi zako zimeshindwa kufua dafu? Tutumie ujumbe kupitia barua pepe, anuani yetu ni

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 07 Dikum Dakum, the magic formula

Author: Ibrahima Ndiaye

lbe@dw-world.de au ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki na vingine vya Noa Bongo tembelea mtandao wetu wa :

www.dw-world.de/lbe.

Hadi wakati mwengine, kwaheri kwa sasa.

END